Ni shahiri na jahara kuwa historia ya fasihi na taaluma za Kiswahli haiwezi kuelezwa bila jina la M.M. Mulokozi kutajwa. Kwa hiyo, inatia moyo sana kuona kitabu hiki cha kumuenzi Profesa huyu; hasa kwa vile aghalabu jadi ya kuwaenzi mashujaa wetu, wawe wa kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii kwa jumla, imekuwa ikihifadhiwa kwa ajili ya waliotutoka tu.

Inatia moyo zaidi kuona kuwa wengi wa wachangiaji katika kitabu hiki ni vijana ambao wameamua kushadidia jadi hii ya kuwaenzi watu waliotoa mchango mkubwa katika maendeleo ya lugha hii kuu ya Afrika na fasihi yake. Ari ya kuona upya fulani katika nyanja mbalimbali za lugha na fasihi ya Kiswahili inajitokeza katika kitabu hiki, hasa kuhusu suala la nadharia. Mathalani, kuhusishwa kwa **Ujumi wa Mtu mweusi** na pia **Ubuntu** kama ilivyofanyika katika Sura ya Tatu ya kitabu hiki ni dalili tosha kuwa vijana wameanza kusaili, kuchokonoa, kulabizi, na kuuliza maswali kuhusu uhalali na ustahiki wa kutumia nadharia ngeni na za nje ya Afrika katika kufanyia tafiti na kuchambulia matokeo ya tafiti hizo za masuala ya Afrika.

Kitabu hiki ni hazina kuu ambayo haitamfanya msomaji amwelewe tu gwiji huyu vizuri zaidi, bali pia ni buku litakalochochea mijadala ya masuala mbalimbali ya fasihi, lugha na utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika katika ngazi mbalimbali shuleni, vyuoni, na kwa wasomaji na watafiti wa kawaida.

F.E.M.K. Senkoro, Profesa wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Namibia, Windhoek, Namibia.

Chapisho hili la kipekee ni mchango maridhawa wa makala za kitaaluma zinazopiga muhuri baraste za kiusomi alizopitia muadhama, mtaalamu na msomi wa Kiswahili, Mugyabuso Mulokozi. Ni makala zinazocheua fikra pevu za wataalamu waliobobea katika tasnia mbalimbali za bahari kuu ya Kiswahili. Ama kwa hakika, zao hili la kitaaluma bila shaka litamlimbua sio tu limbukeni wa taaluma hii bali pia kumjuza mengi mpenzi shadidi wa Kiswahili.

Clara Momanyi, Profesa wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kikatoliki Afrika Mashariki, Kenya.

ISBN: 978 9976 5316 1 9

Kimepigwa Chapa na TUKI
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam


FASIHI, LUGHA NA UTAMADUNI WA KISWAHILI NA KIAFRIKA

Kwa Heshima ya Prof. M.M. Mulokozi

Wahariri:
SHANI OMARI na METHOD SAMWEL

FASIHI, LUGHA NA UTAMADUNI WA KISWAHILI NA KIAFRIKA

Kwa Heshima ya Prof. M.M. Mulokozi



Wahariri

SHANI OMARI na METHOD SAMWEL